TANGAZO LA SERIKALI Na.1002 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA MATOGORO KUSINI KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA MATOGORO KUSINI YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu wa Matogoro Kusini kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Matogoro Kusini ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

**2**. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Matogoro Kusini.

Madhumuni ya tangazo

**3**. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Taifa Matogoro Kusini ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu, nyasi, miti ya miombo na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baianuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

**4**.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao

ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Matogoro Kusini.

Uwasilishaji wa pingamizi

**5**. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza eneo la Msitu Matogoro Kusini kuwa Msitu wa Hifadhi ya Taifa Matogoro Kusini, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

*Tangazo la serikali Na.1002 (linaendelea.)*

**JEDWALI**


*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA SONGEA

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA MATOGORO KUSINI

Makadirio ya eneo: Hekta 3,478.81 au Kilometa za Mraba 34.79 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Matogoro Kusini unaopatikana Wilaya ya Songea katika Mkoa wa Ruvuma kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 3095 (Skeli 1:20,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma,
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*